

mabalozi waliopanda Mlima Kilimanjaro miaka 61 ya Uhuru

# RC awaonya wanaoingiza mifugo Hifadhi ya KINAPA

LILIAN JOEL Na WILLIUM PAUL

**M**KUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, ametangaza kiama kwa majangili wanaoingiza katika Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA).

Aidha, amepiga marufuku wafugaji kuingiza mifugo ndani ya hifadhi kwa sababu inaharibu uoto wa asili na vyanzo vya maji.

Babu alitoa onyo hilo jana, wakati akiwapokea mabalozi wa Tanzania kutoka nchi 11, viongozi wa taasisi za serikali hapanchini na waandiahi wa habari.

Brigedia Jenerali Salum Mnumbe,

aliongoza safari kuipandisha Bendera ya Taifa kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

"Majangili wa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro nawatumia salamu, acheni biashara haramu mnazofanya ndani ya hifadhi, msitake kujua kuwa mimi ni mkuu wa mkoa wa aina gani kwa sababu itawagharimu baba mlinde mwanao," alisema Babu.


Kuhusu wananchi kuingiza mifugo ndani ya hifadhi hiyo, Babu alisema ni marufuku kwa kuwa inaharibu vyanzo vya maji, uoto wa asili na huchangia uwindaji haramu.

"Mifugo yote itakayokamatwa ndani ya hifadhi kuanzia sasa tutaitafisha, kama mtu anajijua ana mifugo afuge siyo kuchunga kiholela hadi ndani ya hifadhi," aliongeza.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) Jenerali mstaafu, George Waitara, alitoa motisha ya sh. milioni tano kwa wapagazi waliobeba mizigo ya watalii hao wa ndani.

Kwa upande wake, Brigedia Jenerali Mnumbe, alitoa rai kwa mkuu huyo wa mkoa, kuhakikisha wapagazi wanajiunga kwenye vikundi na kutafutiwa mashamba katika mikoa mingine ili kujiongezea kipato.

## MIFUGO



DAKTARI wa Mifugo, Paul Ssuna, akitoa elimu kwa wafanyakazi wa Shirika la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT) juu ya kuhudumia mbuzi na kutambua haki za msingi za wanyakwa, Morogoro, Juzi. (Picha na Warioba Igombe).